JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# MWONGOZO WA URATIBU WA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU

AGOSTI 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# MWONGOZO WA URATIBU WA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU

AGOSTI 2025

**MWONGOZO WA URATBU WA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU**

Chapisho hili ni Hakimiliki © ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (OWM-KVAU), Tanzania. Maudhui yaliyomo yanaweza kuzalishwa au kutumika ili kukidhi mahitaji ya Jamii kwa ruhusa ya OWM – KVAU

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ v

**ORODHA YA MICHORO** ........ vi

**VIFUPISHO VYA MANENO** ........ vii

**FASILI YA MANENO** ........ viii

**NENO LA WAZIRI** ........ ix

**DIBAJI** ........ x

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**UTANGULIZI** ........ 1
1.1 Chimbuko ........ 1
1.2 Malengo ya Mwongozo ........ 2
1.2.1 Lengo Kuu ........ 2
1.2.2 Malengo Mahsusi ........ 2
1.3 Walengwa wa Mwongozo ........ 2
1.4 Watumiaji wa Mwongozo ........ 2

**SURA YA PILI** ........ 3

**URATIBU WA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU** ........ 3
2.1 Usajili wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu ........ 3
2.2 Mawasiliano ........ 3
2.3 Maadhimisho ya Watu wenye Ulemavu ........ 4
2.4 Mikutano ya Kimataifa na Kikanda ........ 5
2.5 Uendeshaji wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu ........ 6
2.5.1 Maamuzi Ndani ya Vyama ........ 6
2.5.2 Gharama za Uendeshaji ........ 6

**SURA YA TATU** ........ 7

**MGAWANYO WA MAJUKUMU** ........ 7
3.1 Wizara yenye dhamana na Masuala ya Watu wenye Ulemavu ........ 7
3.1.1 Wizara yenye dhamana na Usajili wa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu ........ 7
3.1.2 Wizara yenye dhamana na Afya ........ 8

3.1.3 Wizara yenye dhamana na Fedha ........ 9
3.1.4 Wizara yenye dhamana na Masuala ya Ustawi wa Jamii ........ 9
3.1.5 Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ........ 9
3.1.6 Sekretarieti za Mikoa ........ 10
3.1.7 Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 10
3.1.8 Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu ........ 11
3.1.9 Vyama vya Watu Wenye Ulemavu ........ 12
3.1.10 Wadau wa Maendeleo na Wadau wa Utekelezaji ........ 12

**SURA YA NNE ........ 13**

**UFUATILIAJI NA TATHIMINI ........ 13**
4.1 Ufuatiliaji na Tathmini ........ 13
4.2 Uandaaji na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji ........ 13
4.3 Kamati za utekelezaji ........ 14
4.4 Gharama za Utekelezaji wa Mwongozo ........ 16
4.5. Mapitio ya Mwongozo ........ 16
4.6. Kuanza Kutumika kwa Mwongozo ........ 16

**VIAMBATISHO ........ 17**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Uandaaji na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji ................................ 16

Jedwali 2: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Taifa................. 16

Jedwali 3: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Mkoa ............... 17

Jedwali 4: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Wilaya.............. 17

Jedwali 5: Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini na Utoaji wa Taarifa .............. 19

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Mfumo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye ulemavu...............7

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **AUL** | Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe |
| **CCSWOP** | Comprehensive Council Social Welfare Operational Plan |
| **MTHUWWU** | Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu wenye Ualbino |
| **NATS** | National Assistive Technology Strategy |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OWM- KVAU** | Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu |
| **PD-MIS** | Persons with Disability Management Information System |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SHIVYAWATA** | Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania |
| **WWU** | Watu wenye Ulemavu |
| **UNCRPD** | United Nations Convention on the Rights of Persons with Disabilities |

## FASILI YA MANENO

| | |
|---|---|
| **Marekebisho** | Ina maana ya huduma za marekebisho ni jumla ya juhudi za pamoja katika nyanja za afya, saikolojia, elimu, ufundi, kazi na jamii zenye madhumuni ya kuinua kiwango cha utendaji wa Mtu mwenye Ulemavu kwa kiasi kinachomwezesha kushiriki kwa ukamilifu katika maisha ya kila siku ya jamii yake. |
| **Matawi** | Ina maana ya tawi la msingi la wanachama ambalo litakuwa na wanachama waliomo katika Mtaa, Kijiji, Kata, Tarafa au taasisi. |
| **Mtu mwenye ulemavu** | Ina maana ya Mtu mwenye changamoto ya kimwili, kisaikolojia, kiakili au kihisia ambaye uwezo wake wa viungo kufanya kazi unazuia ushiriki wake kamili na ufanisi katika jamii kutokana na mazingira na vikwazo mbalimbali. |
| **Shirikisho** | Ina maana ya Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria. |
| **Shirika lisilo la Kiserikali** | Ina maana ya kikundi binafsi na cha hiari cha watu au mashirika, chenye dhamira ya kukuza malengo halali ya kiuchumi, kijamii au kiutamaduni, kinachoanzishwa kwa mujibu wa Sheria kwa lengo la kuisaidia jamii. |
| **Utengamao** | Ina maana ya urejeshaji wa utimamu wa kimwili na kiakili wa Mtu mwenye Ulemavu ili kumwezesha kumudu mazingira yanayomzunguka. |
| **Vyama** | Ina maana ya Vyama vya Watu wenye Ulemavu vilivyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria. |

# NENO LA WAZIRI



Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika masuala ya utoaji maamuzi yanayohusu haki na ustawi wao kama ilivyobainishwa kupitia Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sura 183 pamoja na Sheria ya Vyama vya Kijamii Sura 337. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) na Vyama Shiriki na kwa nia ya kuendeleza na kukuza haki na ustawi wa Watu wenye Ulemavu, imeridhia Mikataba ya Kimataifa na kikanda ikiwemo UNCRPD (2006) na Itifaki ya SADC (2024).

Vilevile, imeandaa mipango, mikakati na programu ikiwemo Malengo Endelevu ya Maendeleo (2030), MTHUWWU (2024), NATS (2024), Mikopo isiyokuwa na riba ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri na PD-MIS (2023) lengo likiwa ni kukuza ustawi wa Watu wenye Ulemavu.

Pamoja na jitihada hizi za Serikali, bado kumekuwa na changamoto ya uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu katika ngazi ya Serikali za Mitaa, Tawala za Mikoa na Serikali Kuu hususan katika maeneo ya mawasiliano, uendeshaji na usimamizi wa Vyama hivyo. Changamoto hizi zimeilazimu Serikali kuandaa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2025 ambao unahitaji kuzingatiwa na Wadau wote ili kuimarisha utendaji wa Vyama husika hali itakayoviwezesha kuwa na ustawi.

Hivyo, natoa wito kwa Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Wizara za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, Wadau wa Utekelezaji, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Jamii kushirikiana kikamilifu ili kuhakikisha Mwongozo huu unatekelezwa kama ilivyokusudiwa ili kuimarisha ustawi kwa Watu wenye Ulemavu nchini.

Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)**

# DIBAJI



Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu ni chachu katika kuleta ustawi na maendeleo endelevu ya Vyama na Wanachama wao nchini. Katika jitihada za kuwa na sauti ya pamoja katika kushughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu, Vyama vya Watu wenye Ulemavu vilianzisha Shirikisho lao. Pamoja na kuwa na Shirikisho, uendeshaji wa Vyama umeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa hususan katika eneo la uratibu. Kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha uendeshaji wa Vyama, Serikali imeandaa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2025 ambao utekelezaji wake utaviwezesha Vyama, Serikali na Wadau kufikia malengo waliyojiwekea katika utoaji huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

Uandaaji wa Mwongozo umeshirikisha wadau muhimu wakiwemo, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Serikali, Sekta Binafsi na Wadau wengine katika Sekta ya Ustawi wa Jamii. Serikali inatoa shukrani za dhati kwa wadau waliotoa maoni yaliyowezesha kuandaliwa kwa Mwongozo huu.

Mwongozo huu unatoa utaratibu utakaozingatiwa na Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Shirikisho, Mamlaka za Serikali, Wadau wa Maendeleo, Wadau wa Utekelezaji na Sekta Binafsi ili kuimarisha ufanisi katika uendeshaji wa Vyama hali itakayoondoa migongano ya kimaslahi inayoweza kusababisha migogoro isiyo ya lazima, hivyo kudhoofisha utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu. Serikali kwa kushirikiana na Wadau, itahakikisha malengo ya Mwongozo huu yanafikiwa kwa wakati.

Mary N. Maganga
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Mwongozo wa uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu unaweka utaratibu madhubuti utakaohakikisha Vyama vinatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera, Sheria na Miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa inayohusiana na haki na ustawi wa Watu wenye Ulemavu.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Sera; Sheria hususani Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2004, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sura ya 183 na Sheria ya Vyama vya Kijamii, Sura ya 337; Mikataba ya Kikanda na Kimataifa hususan Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2006 (UNCRPD); na Sera ya Watu wenye Ulemavu ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2012 pamoja na maoni ya wadau.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuratibu Vyama vya Watu wenye Ulemavu kulingana na aina ya Ulemavu wao pamoja na umoja wa Vyama hivyo unaojulikana kwa jina la Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) na wadau wengine wanaoshirikiana na Vyama na Shirikisho. Hadi wakati wa uandaaji wa mwongozo huu, Tanzania ina jumla ya Vyama vya Watu wenye Ulemavu 12 na Shirikisho moja (1).

### 1.1 Chimbuko

Serikali imeandaa mifumo ya haki na ustawi wa Watu wenye Ulemavu ili kuleta ushiriki, ushirikishwaji na uwezeshwaji wao kupitia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayohusu ustawi wa Watu wenye Ulemavu, kama vile Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu (2004), Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura ya 183 na Kanuni zake. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Wadau imeendelea kutekeleza programu, mikakati na mipango mbalimbali kama vile Mkakati wa Teknolojia Saidizi wa Mwaka 2024 – 2027 (NATS), Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu wenye Ualbino 2024/2025 – 2028/2029 (MTUHWWU) na Mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri.

Pamoja na jitahada hizo, bado kuna changamoto katika uratibu wa masuala ya Vyama vya Watu wenye Ulemavu katika ngazi ya Serikali za Mitaa, Tawala za Mikoa na Serikali Kuu hususan katika maeneo ya uendeshaji na usimamizi wa Vyama hivyo. Kumekuwa na mawasiliano yasiyozingatia mamlaka ya kiutawala, gharama kubwa za ushiriki na uendeshaji wa maadhimisho ya vyama vya Watu wenye Ulemavu na migogoro ya mara kwa mara ndani ya vyama na kati ya chama na chama hali inayosababisha ufanisi mdogo katika kuwahudumia wanachama wao. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali imeona

upo umuhimu wa kuandaa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2025 ili kuimarisha uendeshaji wa Vyama, hivyo na kufikia malengo katika kuwahudumia wanachama wao.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

### 1.2.1 Lengo Kuu

Kuweka uratibu madhubuti wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu ili kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazohusu haki na ustawi wa Watu wenye Ulemavu.

### 1.2.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi yanayotokana na lengo kuu la kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu Vyama vya Watu wenye Ulemavu ni-

(a) Kuimarisha mfumo wa uratibu wa Vyama, Wadau na Serikali, ili kuongeza tija, ufanisi na usawa katika utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu;
(b) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa Vyama katika kuwahudumia wanachama wao;
(c) Kukuza uelewa miongoni mwa wanachama na wadau kuhusu masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(d) Kuimarisha utendaji wa Vyama na Wadau katika ngazi mbalimbali katika kushughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(e) Kuhamasisha Vyama kujitegemea kimaendeleo na kuwa na mipango ya maendeleo endelevu kwa ustawi wa Vyama na wanachama; na
(f) Kuhakikisha kila mdau anafanya ufuatiliaji na tathmini endelevu juu ya utendaji wa Vyama katika eneo lake la kiutawala ili kubaini mafanikio, changamoto na kuchukua hatua za kuimarisha utendaji ili kufikia malengo tarajiwa.

### 1.3 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu unalenga Vyama vya Watu wenye Ulemavu na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu.

### 1.4 Watumiaji wa Mwongozo

Watumiaji wa Mwongozo ni Wizara yenye dhamana na uratibu wa masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Wizara za Kisekta, Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wengine na wadau wengine kulingana na mahitaji.

# SURA YA PILI

## URATIBU WA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU

Uratibu wa Vyama unahusisha usajili, mawasiliano, maadhimisho, mikutano na uendeshaji. Uratibu huu umechanganuliwa kwa kila kipengele kama ilivyoanishwa. Pia Mchoro Na.1 umeonesha namna uratibu huu utafanyika kuanzia ngazi ya Vyama hadi Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu.

### 2.1 Usajili wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu

Mashirika au Vyama vya Kijamii huanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura 337. Kwa muktadha huo, usajili wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu utaendelea kufanyika kupitia Msajili wa Vyama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mwongozo huu, Chama kitakachoratibiwa ni chenye sifa zifuatazo-

(a) Kiwe na Katiba iliyoainisha: Wasifu na majukumu ya viongozi, Vyanzo vya mapato, taratibu za Uwazi na Uwajibikaji, Muundo wa uendeshaji unaolingana na uwezo wa Chama (Organogram), Mfumo wa utatuzi wa migogoro unaoheshimu sheria, Kutambua uanachama wao kwenye Shirikisho, Uzingatiaji wa uwiano wa kijinsia, Kulinda haki za watoto, vijana na wazee na Mfumo wa mawasiliano unaotambua Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(b) Kiwe na mipango ya maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu;
(c) Kiwe na Cheti cha uthibitisho wa aina ya ulemavu kutoka Wizara ya Afya; na
(d) Kiwe na tamko la kulinda haki za Watoto.

Usajili wenye kuzingatia vigezo hivyo utasaidia kuweka uwazi, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa Vyama vya Watu wenye Ulemavu vinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

### 2.2 Mawasiliano

Mawasiliano katika uendeshaji wa Vyama ni muhimu kwa kuwa yanawezesha uratibu ili kuleta uwazi na kuweka mipaka ya kiutendaji, uwajibikaji, ushirikiano na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Vyama.

Kwa mujibu wa Mwongozo huu, mawasiliano yanaanza ngazi ya Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu; hali kadhalika, kwa upande wa Vyama, mawasiliano yanaanza kwa mwanachama ngazi ya Tawi hadi Viongozi ngazi ya Taifa. Kupitia Mwongozo huu njia za mawasiliano ni:

(a) **Mikutano rasmi na mashauriano ya mara kwa mara**: Itatumika na Vyama na Shirikisho kujadili masuala ya kuimarisha huduma kwa ajili ya ustawi wa wanachama wao;

(b) **Mifumo ya mawasiliano**: Matumizi ya tovuti rasmi, majarida, vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii yatatumika kwa ajili ya kutoa taarifa rasmi, kubadilishana maoni na kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali, Vyama na Wadau;

(c) **Warsha na Mafunzo**: Zitatumika kujenga uelewa kuhusu uendeshaji na uratibu wa Vyama kwa viongozi, wanachama pamoja na wadau;

(d) **Vikao vya Ushirikiano vya Wadau**: Vitafanyika katika ngazi zao za kiutawala ili kujadili masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu kwa nia kuimarisha ushirikiano baina yao;

(e) **Taarifa za Utekelezaji:** Zitawasilishwa kila robo mwaka na mwaka kwa wadau katika ngazi mbalimbali za kiutawala ili kufahamu **mwenendo** wa utekelezaji, mafanikio, changamoto na utatuzi wake; na

(f) **Ngazi za mawasiliano:** Vyama na Wanachama vitawasilisha masuala yao kwa kufuata ngazi za kiutawala kama inavyoonekana katika Mchoro Na.1 wa Mwongozo huu. Aidha, mawasiliano baina ya Chama na Serikali au Wadau wa Maendeleo na Wadau wa Utekelezaji yatapita kwenye Shirikisho.

## 2.3 Maadhimisho ya Watu wenye Ulemavu

Maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu yamekuwa yakiadhimishwa katika ngazi ya Kitaifa. Hata hivyo, ushiriki wa wanachama wa Vyama umekuwa hafifu kutoka katika maeneo yao kwa sababu mbalimbali hali inayosababisha maadhimisho hayo kukosa tija. Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kufanyika kwa maadhimisho haya kama ifuatavyo:

**(a) Ngazi ya Halmashauri**

Maadhimisho mahsusi ya Vyama kwa aina ya ulemavu kwa Mwongozo huu yafanyike ngazi ya Halmashauri zote nchini. Aidha, chama husika kitamuomba Mkurugenzi wa Halmashauri moja wapo kuwa mwenyeji Kitaifa. Wanachama wa chama kinachoadhimisha kwa Mwongozo huu watashiriki katika Halmashauri zao. Chama kitaratibu maadhimisho mahsusi, ambapo gharama za maadhimisho hayo zitaandaliwa kwa ushirikiano baina ya chama husika, Halmashauri na Wadau. Kuhusu maadhimisho mawili yanayolenga aina moja ya ulemavu, maadhimisho hayo yaunganishwe na yafanyike kwa tarehe moja ya kitaifa itayoafikiwa kupitia SHIVYAWATA. Vile vile, chama hicho kitahusika kuratibu maadhimisho hayo kwa kushirikiana na Halmashauri mwenyeji. Wageni Rasmi katika maadhimisho mahsusi ya Vyama watatafutwa na uongozi wa vyama husika. Aidha, Waziri mwenye dhamana atatoa tamko kupitia vyombo vya habari kutambua umuhimu wa siku hiyo ya kimataifa.

**(b) Ngazi ya Kitaifa**

Kwa mujibu wa Mwongozo huu kutakuwa na Wiki ya Watu wenye Ulemavu ya Kitaifa ambayo kilele chake kitakuwa tarehe 3 Desemba ya kila mwaka ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani. Wiki hii

itahusisha Vyama na wanachama wao kutoka Mikoa yote Tanzania Bara. Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya atakuwa miongoni mwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Maadhimisho ngazi ya Taifa yataratibiwa na SHIVYAWATA kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya uratibu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu, OR-TAMISEMI, Wizara za Kisekta, na Wadau wengine muhimu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu.


### 2.4 Mikutano ya Kimataifa na Kikanda

Mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayotambulika na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda ikiwemo ile ambayo inatokana na utekelezaji wa Mikataba iliyoridhiwa na nchi itaratibiwa kama ifuatavyo:

(a) **Mkutano mahsusi kwa aina ya ulemavu**: Itaratibiwa na Chama husika kwa kusimamiwa na Shirikisho pamoja na Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu; na

(b) **Mikutano ya jumla:** Itaratibiwa na Shirikisho kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu na Wadau.

**Mchoro Na.1: Mfumo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu**



## 2.5 Uendeshaji wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu

Uendeshaji wa Vyama utazingatia Katiba zinazoanzisha Vyama hivyo pamoja na Sheria, Kanuni na Miongozo ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu masuala tajwa. Pia, uendeshaji wa Vyama utahusisha utekelezaji wa kazi za kila siku na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa ufanisi.

### 2.5.1 Maamuzi Ndani ya Vyama

Mwongozo unaelekeza Vyama kuzingatia masuala ya msingi vinapofanya maamuzi kuhusu masuala ya uendeshaji. Maamuzi yazingatie masuala ya msingi yafuatayo ili kuleta utulivu na amani ndani ya Vyama:

(a) **Katiba:** Maamuzi yatakayofanyika ndani ya Vyama yazingatie Katiba za Vyama na Shirikisho;
(b) **Utawala wa Sheria** Maamuzi yazingatie Sheria zilizopo;
(c) **Uwazi na Uwajibikaji:** Yazingatie taratibu za utoaji wa taarifa za maamuzi kwa wanachama wake na kuwajulisha hatua zilizochukuliwa ili kuonesha uwajibikaji;
(d) **Ushiriki na Ushirikishwaji:** Uwepo wa mazingira wezeshi kwa wanachama na viongozi kushiriki katika maamuzi yaliyofikiwa;
(e) **Uwiano wa kijinsia:** Uwepo wa utaratibu wa ujumuishwaji wa usawa wa kijinsia katika utoaji wa maamuzi;
(f) **Maamuzi kuhusu Mali za Chama:** Yashirikishe uongozi wa Chama kwa ujumla wake pamoja na Mamlaka za Kiutawala katika eneo husika; na
(g) **Utatuzi wa Migogoro:** Vyama viweke mfumo wa utatuzi wa migogoro ulio wazi na vitambue Shirikisho na Mamlaka za kiutawala katika maeneo husika kama mamlaka za rufaa za migogoro hiyo.

### 2.5.2 Gharama za Uendeshaji

Vyama vitaendesha shughuli zake kwa uwazi na kuzingatia mipango na mikakati iliyojiwekea inayozingatia vipaumbele vya Serikali. Uendeshaji wa Vyama unapaswa kuzingatia taratibu za fedha zilizopo. Hivyo, Vyama vina wajibu wa kubainisha:

(a) Vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wake, uchaguzi wa viongozi wa vyama na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(b) Mipango ya muda mfupi, kati na mrefu na kuweka vigezo vya kupima utekelezaji na mafanikio ya shughuli zinazofanyika;
(c) Taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wanachama na wadau;
(d) Matumizi ya teknolojia ya kidigitali kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji, uchaguzi wa viongozi wa vyama, mawasiliano na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na
(e) Mipango na bajeti za Vyama kwa kazi za kisekta, kitaasisi na kiidara/ kitengo ili kuhakikisha kuwa malengo na shughuli zinatekelezwa kwa ufanisi.

# SURA YA TATU

## MGAWANYO WA MAJUKUMU

Mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji wa Mwongozo huu utahusisha, Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara za Kisekta, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vyama, Shirikisho, Wadau wa Maendeleo na Wadau wa Utekelezaji.

### 3.1 Wizara yenye dhamana na Masuala ya Watu wenye Ulemavu

Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu;
(b) Kuratibu utekelezaji wa Mikataba na Itifaki za Kimataifa, Kikanda na Afrika Mashariki kuhusu Vyama na wanachama;
(c) Kutoa elimu kwa umma juu ya uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu;
(d) Kufanya uchambuzi na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mbinu za kuzuia kuongezeka kwa ulemavu;
(e) Kupitia taarifa za utekelezaji za Vyama zilizowasilishwa na Shirikisho;
(f) Kuandaa na kuratibu mipango endelevu kuhusiana na Vyama;
(g) Kuratibu tafiti endelevu kuhusu ulemavu na masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(h) Kufanya uchambuzi na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Shirikisho kuhusu upatikanaji wa huduma kwa wanachama wake;
(i) Kuratibu vikao kati ya Wizara yenye dhamana, Wizara za kisekta, Wadau wa Maendeleo na Wadau wa Utekelezaji wa Programu za Kitaifa kuhusu masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Shirikisho;
(j) Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu;
(k) Kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani tarehe 03 Desemba ya kila mwaka; na
(l) Waziri mwenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu atatoa tamko la kutambua maadhimisho mahsusi ya Vyama Kimataifa.

#### 3.1.1 Wizara yenye dhamana na Usajili wa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu

Wizara yenye dhamana na usajili wa Vvyama vya Watu wenye Ulemavu itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kusajili Vyama vya Watu Wenye Ulemavu kwa kuzingatia taarifa ya uthibitisho wa aina ya Ulemavu kutoka Wizara ya Afya;
(b) Kuvifuta vyama vile ambayo vimekiuka masharti ya usajili kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura 337;

(c) Kufanya usajili wa Chama kimoja (1) kwa kila aina ya ulemavu;
(d) Kuzingatia masuala yaliyoainishwa katika Kipengele **Na. 2.1.** cha Mwongozo huu katika kusajili Vyama;
(e) Atakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu usajili, uendeshaji na utatuzi wa migogoro ya Vyama;
(f) Kutoa elimu kuhusu usajili na utekelezaji wa masharti ya usajili ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(g) Kuteua Maafisa wa Serikali (Wasajili Wasaidizi) ngazi ya Mkoa na Halmashauri ambao watakuwa wanatekeleza majukumu yao ya usajili, ufuatiliaji, utoaji elimu na uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu chini ya Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337;
(h) Kuchambua taarifa za utekelezaji za robo mwaka, taarifa za utekelezaji na taarifa za ukaguzi za mwaka za Vyama vya Watu wenye Ulemavu;
(i) Kuchambua taarifa za utendaji wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu kutoka OR - TAMISEMI;
(j) Kujenga uwezo kwa Wasajili Wasaidizi (Maafisa Ustawi wa Jamii) ngazi ya Mkoa na Halmashauri pamoja na Vyama vya Watu wenye Ulemavu ili kuweza kuboresha utendaji kwa kufuata Sheria, Kanuni, taratibu na maadili ya nchi;
(k) Kuhakikisha kuwa mikataba ya ufadhili wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu inawasilishwa kwa Msajili wa Jumuiya za Kiraia ili kujenga dhana ya uwazi na uwajibikaji;
(l) Kufanya ufuatiliaji ngazi ya Mkoa na Halmashauri wa utekelezaji wa masharti ya usajili na uendeshaji wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura 337;
(m) Kutoa Kanuni, Miongozo na Taratibu za uendeshaji wa Vyama ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri; na
(n) Kukusanya, kutunza, na kusambaza taarifa za Vyama.

### 3.1.2 Wizara yenye dhamana na Afya

Wizara yenye dhamana na afya itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) Kutambua na kuthibitisha Ulemavu;
(b) Kusimamia na kushauri juu ya ubora wa vifaa saidizi kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na Watu wenye Ulemavu
(c) Kutoa elimu ya matokeo ya tafiti na tathmini zinazohusiana na visababishi vya ulemavu kwa Vyama na Wadau wa masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(d) Kutoa na kusambaza Miongozo ya Utoaji wa Huduma za Mkoba, Kliniki Bobezi, Huduma za Utengamao na Vifaa Saidizi na Miongozo mingine kwa kushirikiana na Vyama; na
(e) Kushiriki Mikutano ya Kimataifa, Kikanda, Afrika Mashariki na Kitaifa inayohusu masuala ya afya kwa Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Vyama.

### 3.1.3 Wizara yenye dhamana na Fedha

Wizara yenye dhamana na fedha itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kuratibu upatikanaji wa fedha za ruzuku kwa ajili ya kuviwezesha Vyama; na

(b) Kutoa Miongozo ya Mipango na Bajeti inayojumuisha masuala ya Watu wenye Ulemavu.

### 3.1.4 Wizara yenye dhamana na Masuala ya Ustawi wa Jamii

Wizara yenye dhamana na masuala ya ustawi wa jamii itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kushirikiana na Vyama kuratibu masuala ya huduma na makazi kwa Watu wenye Ulemavu wasiojiweza;

(b) Kushirikiana na Vyama katika kuwaunganisha Watu wenye Ulemavu wenye uhitaji na walezi, ndugu au jamii;

(c) Kutoa huduma ya utengamao ngazi ya jamii kwa kushirikiana na Shirikisho;

(d) Kusimmamia utoaji wa huduma ya matunzo na uangalizi kwa Watu wenye Ulemavu katika Magereza, Mahabusu na Taasisi za Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Vyama; na

(e) Kushiriki Mikutano ya Kimataifa, Kikanda, Afrika Mashariki na Kitaifa inayohusu huduma na matunzo kwa Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Vyama.

### 3.1.5 Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wizara yenye dhamana na tawala za mikoa na serikali za mitaa itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kukuza uelewa kwa Vyama na wanachama wao kuhusu wajibu na majukumu ya Wizara katika kuwahudumia;

(b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(c) Kupokea na kuchambua taarifa za utekelezaji za Vyama zilizowasilishwa na Sekretarieti za Mikoa;

(d) Kuratibu Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na Masuala ya Watu wenye Ulemavu, Shrikisho na Wadau wa wengine;

(e) Kuratibu Maadhimisho ya Kimataifa mahsusi ya Vyama kwa aina ya ulemavu katika Halmashauri kwa kushirikiana na Vyama na Wadau wengine;

(f) Kuandaa na kuratibu mipango endelevu ya kujengea uwezo Vyama kupitia CCSWOP kwa kushirikiana na Shirikisho;

(g) Kuratibu na kutatua migogoro ya wanachama na Vyama katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(h) Kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Shirikisho kuhusu upatikanaji wa huduma kwa wanachama wake.

**3.1.6 Sekretarieti za Mikoa**

Sekretarieti za Mikoa zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kukuza uelewa kwa Vyama na wanachama wao kuhusu wajibu na majukumu ya Serikali za Mitaa katika kuwahudumia Watu wenye Ulemavu;
(b) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali kuhusu Watu wenye Ulemavu;
(c) Kuhakikisha masuala ya Watu wenye Ulemavu yanapewa kipaumbele katika mipango ya maendeleo ya Mikoa na Halmashauri kupitia CCSWOP;
(d) Kuratibu na kutatua migogoro ya wanachama na Vyama katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(e) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uendeshaji wa Vyama ili kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
(f) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Vyama kwenye Kamati ya Watu wenye Ulemavu ya Mkoa kabla ya kuwasilishwa OR –TAMISEMI;
(g) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Vyama katika Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia mifumo ya CCSWOP na PD-MIS baada ya utekeleaji wa kipengele cha 3.1.6 (f); na
(h) Kushiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani Desemba ya kila Mwaka.

**3.1.7 Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kutambua na kusajili Wanachama na Matawi ya Vyama kupitia PD-MIS katika Mitaa/Vijiji/Taasisi kwa kushirikiana na Vyama;
(b) Kutekeleza Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu;
(c) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Vyama kwenye Kamati ya Watu wenye Ulemavu ya Halmashauri kabla ya kuwasilishwa Sekretarieti ya Mkoa;
(d) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji za Vyama vilivyo katika maeneo yao ya kiutawala kwa Sekretarieti ya Mkoa baada ya utekelezaji wa Kipengele cha 3.1.7 (c);
(e) Kuandaa na kutekeleza mipango endelevu ya kujengea uwezo Vyama na wanachama wake;
(f) Kufanya uchunguzi wa visababishi vya ongezeko la ulemavu na matukio ya ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mamlaka katika maeneo yake;
(g) Kutoa Huduma za Mkoba na Vifaa Saidizi kwa Watu wenye Ulemavu katika Mtaa/Vijiji kwa kushirikiana na Vyama;
(h) Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya uendeshaji wa Vyama;

(i) Kuandaa na kuadhimisha maadhimisho ya Kimataifa mahsusi kwa aina ya ulemavu kwa kushirikiana na Vyama na Wadau wa Utekelezaji katika maeneo yao ya Kiutawala; na
(j) Kuwezesha ushiriki wa Watu wenye Ulemavu na wataalam kutoka Halmashauri yake kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani Desemba ya kila Mwaka.

**3.1.8 Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu**

Shirikisho litakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) Kuwa kiungo kati ya Vyama na Wizara yenye dhamana ya Watu wenye Ulemavu, Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara za Kisekta na Wadau wa masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(b) Kuandaa vikao vya kiutendaji na Vyama wanachama na kupokea taarifa za utekelezaji;
(c) Kushiriki na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Vyama katika vikao vya nusu mwaka na mwaka kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(d) Kusajili Wanachama wake kwa kuwasiliana na Mamlaka yenye dhamana ya usajili wa Vyama;
(e) Kuwa chombo cha utatuzi wa migogoro ya wanachama wake;
(f) Kutoa rufaa kwenda kwa Msajili wa Jumuiya za Kiraia kwa migogoro iliyoshindwa kutatuliwa na Shirikisho;
(g) Kuwasilisha taarifa ya ukaguzi wa fedha za Shirikisho na Vyama wanachama kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(h) Kuvijengea uwezo Vyama wanachama kuhusu utekelezaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(i) Kuongeza uelewa wa jamii juu ya haki, mahitaji na ustawi wa Watu wenye Ulemavu;
(j) Kujumuisha masuala ya Makundi Anuwai wakiwemo Wanawake, Vijana, Wazee na Watoto wenye Ulemavu katika utekelezaji wa majukumu yake;
(k) Kuratibu ushiriki wa Vyama katika Mikutano ya Kimataifa, Kikanda, Afrika Mashariki na Kitaifa inayohusu masuala ya Watu wenye Ulemavu;
(l) Kuratibu Maadhimisho ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu pamoja Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
(m) Kuratibu Maadhimisho ya Kimataifa mahususi kwa aina ya ulemavu katika Halmashauri kwa kushirikiana na Vyama, OR-TAMISEMI na Wadau wengine; na
(n) Kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuendesha shughuli za vyama.

### 3.1.9 Vyama vya Watu Wenye Ulemavu

Vyama vitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kuwa kiungo kati ya Watu wenye Ulemavu, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mtaa na Shirikisho;
(b) Kusajili wanachama na kuhakikisha wanaingizwa kwenye Mfumo wa PD-MIS;
(c) Kuratibu Maadhimisho ya Kimataifa mahususi kwa aina ya ulemavu katika ngazi ya Halmashauri kwa kushirikiana na Shirikisho;
(d) Kuweka utaratibu wa kutatua migogoro ndani ya Vyama;
(e) Kutoa rufaa kwenda kwa Shirikisho kwa migogoro iliyoshindwa kutatuliwa na Chama;
(f) Kuwasilisha taarifa ya ukaguzi wa fedha katika Shirikisho na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(g) Kuandaa taarifa za utekelezaji na kuwasilisha katika Shirikisho na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(h) Kutatua changamoto zinazowakabili wanachama wake kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shirikisho; na
(i) Kuandaa vipaumbele kwa ajili ya kuzingatiwa katika maandalizi ya Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 3.1.10 Wadau wa Maendeleo na Wadau wa Utekelezaji

Wadau wa Maendeleo na Utekelezaji watakuwa na majukumu yafuatayo:

#### 3.1.10.1 Wadau wa Maendeleo

(a) Kutoa ushauri wa kitaalamu na fedha ili kuwezesha utekelezaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu; na
(b) Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya Miradi na Programu wanazozifadhili.

#### 3.1.10.2. Wadau wa Utekelezaji

(a) Kushirikiana na Serikali katika kutekeleza masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu;
(b) Kutekeleza miradi na programu zinazohusu Watu wenye Ulemavu na Vyama vyao; na
(c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na Serikali.

# SURA YA NNE

## UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 4.1 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu utafanyika kwa ngazi nne (4) kwa kuzingatia maeneo ya Uongozi na Utawala bora; Mipango na Bajeti; na Ushiriki na Ushirikishwaji kama ifuatavyo:

(a) OWM-KVAU itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo kwa Shirikisho, OR-TAMISEMI na Wizara za Kisekta mara moja kwa mwaka;

(b) OR-TAMISEMI itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo kwa SHIVYAWATA, Sekretarieti za Mikoa na Wadau wa Utekelezaji mara moja kwa mwaka;

(c) Sekretarieti za Mikoa zitafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo kwa SHIVYAWATA Mkoa, Halmashauri na Wadau wa Utekelezaji mara mbili kwa mwaka; na

(d) Mamlaka za Serikali za Mitaa zitafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo kwa Vyama na Wadau wa Utekelezaji katika maeneo yao ya kiutawala kila robo mwaka.

Utekelezaji wa Mwongozo utafuatiliwa katika vipindi tofauti na kufanyiwa tathmini kwa kipindi cha miaka mitano (5) au pale itakavyoonekana kuna uhitaji ili kupima kiwango cha utekelezaji wa Mwongozo.

Vyama vinapaswa kujifanyia tathmini kila mwaka ili kubaini mafanikio na changamoto zilizotokana na uratibu na uendeshaji wake. Ili kuweza kufanikisha kufanyika kwa tathmini zenye matokeo, Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu itafanya zoezi la kukusanya taarifa za awali za utekelezaji wa Mwongozo kwa kushirikiana na Wadau.

### 4.2 Uandaaji na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Wizara za Kisekta, OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau watawasilisha taarifa za utekelezaji kwa lengo la kupima mafanikio, kubaini changamoto na kuweka mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa masuala yanayohusu Watu wenye Ulemavu. Wadau tajwa wanapaswa kuandaa taarifa za utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia utaratibu uliooneshwa kwenye **Jedwali Na.1** lifuatalo:

**Jedwali 1: Uandaaji na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji**

| Na. | Mhusika | Muda wa Kuwasilisha | Mahali pa Kuwasilisha |
|---|---|---|---|
| 1. | Vyama vya Watu wenye Ulemavu ngazi ya Wilaya | Robo Mwaka | Halmashauri |
| 2. | Halmashauri | Robo mwaka | Sekretarieti ya Mkoa |
| 3. | Sekretariet za Mikoa | Robo Mwaka | Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. |
| 4. | OR - TAMISEMI | Mwaka | Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu |
| 5. | Wizara za Kisekta | Mwaka | Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu |
| 6. | Vyama ngazi ya Taifa | Robo | Shirikisho |
| 7. | Shirikisho | Nusu Mwaka | Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu |

### 4.3 Kamati za utekelezaji

Mwongozo huu utatekelezwa kupitia Kamati katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri ambapo Kamati ya Taifa, itakutana mara moja kwa mwaka. Aidha, Kamati katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri katika Mwongozo huu ina maana ya Kamati za Watu wenye Ulemavu zilizopo ngazi ya Mkoa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sura 183 na uitishwaji wa vikao vyake utazingatia Sheria hiyo. Orodha ya Wajumbe wa Kamati ni kama ilivyooneshwa kwenye **Majedwali Na. 2 hadi 4** yafuatayo:

**Jedwali 2: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Taifa**

| Na. | Mhusika | Ofisi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Katibu Mkuu | OWM-KVAU | Mwenyekiti |
| 2. | Mwenyekiti | SHIVYAWATA | Mwenyekiti Mwenza |
| 3. | Katibu Mkuu | SHIVYAWATA | Mjumbe |
| 4. | Wawakilisha wa Vyama wanachama wa SHIVYAWATA wawili (2) kwa kuzingatia jinsi | SHIVYAWATA | Wajumbe |
| 5. | Mkuu wa Kitengo cha Sheria | OWM-KVAU | Mjumbe |

| Na. | Mhusika | Ofisi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 6. | Mkurugenzi anaehusika na Masuala ya Ustawi wa Jamii | OR-TAMISEMI | Mjumbe |
| 7. | Kamishna wa Ustawi wa Jamii | WMJJWM | Mjumbe |
| 8. | Msajili wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu | Mambo ya Ndani ya Nchi | Mjumbe |
| 9. | Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu wenye Ulemavu | OWM-KVAU | Katibu |

**Jedwali 3: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Mkoa**

| Na. | Mhusika | Ofisi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Mteule wa Mkuu wa Mkoa | Mkoa | Mwenyekiti |
| 2. | Katibu Tawala (M) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Mjumbe |
| 3. | Katibu Tawala Msaidizi (AUL) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Mjumbe |
| 4. | Mkuu wa Kitengo cha Sheria | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Mjumbe |
| 5. | Mwakilishi wa Wabunge | Mkoa | Mjumbe |
| 6. | Mwakilishi SHIVYAWATA | SHIVYAWATA (M) | Mjumbe |
| 7. | Wawakilishi wawili 2 kutoka katika Vyama | Vyama (M) | Mjumbe |
| 8. | Mdau kutoka Taasisi zinazohudumia WWU | Mdau (M) | Mjumbe |
| 9. | Afisa U/Jamii (M) | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Katibu |

**Jedwali 4: Orodha ya Wajumbe wa Kamati katika Ngazi ya Wilaya**

| Na. | Mhusika | Ofisi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Mteule wa Mkuu wa Wilaya | Wilaya | Mwenyekiti |
| 2. | Mkurugenzi wa Halmashauri | Ofisi ya Mkurugenzi | Mjumbe |
| 3. | Mkuu wa Idara ya AUL | Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri | Mjumbe |
| 4. | Mkuu wa Kitengo cha Sheria | Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri | Mjumbe |
| 5. | Mbunge wa Jimbo | Halmashauri | Mjumbe |
| 6. | Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii | Halmashauri | Mjumbe |

| Na. | Mhusika | Ofisi | Nafasi |
|---|---|---|---|
| 7. | Mwakilishi wa SHIVYAWATA | SHIVYAWATA (W) | Mjumbe |
| 8. | Mwakilishi mmoja (1) kutoka katika Vyama | Vyama (W) | Mjumbe |
| 9. | Mdau kutoka Taasisi zinazohudumia WWU | Mdau (W) | Mjumbe |
| 10. | Wawakilishi wawili (2) kutoka kwenye jamii kwa kuzingatia Jinsi | Halmashauri | Wajumbe |
| 11. | Afisa U/Jamii (Halmashauri) | Ofisi ya Mkurugenzi - Halmashauri | Katibu |

### 4.4 Gharama za Utekelezaji wa Mwongozo

Gharama za utekelezajii wa Mwongozo wa Uratibu wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu zitakuwa ni za Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa Mwongozo huu kulingana na majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo.

### 4.5. Mapitio ya Mwongozo

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu au kadri itakavyohitajika ili kukidhi mabadiliko katika Sera, Sheria na Kanuni na mambo mengi yatakayojitokeza.

### 4.6. Kuanza Kutumika kwa Mwongozo

Mwongozo huu utaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Mamlaka zinazohusika.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na.1**

**Jedwali 5: Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini na Utoaji wa Taarifa**

| Eneo | Viashiria | Viashiria vya Uthibitishaji | Wahusika |
|---|---|---|---|
| **Usajili wa Vyama** | Idadi ya Vyama vilivyojisajili na kufuatiliwa kwa mujibu wa Mwongozo | Taarifa za usajili na ukaguzi wa taarifa za Vyama | Msajili wa Vyama |
| **Ushiriki wa Vyama katika Shughuli za Maendeleo** | Idadi ya afua zilizotekelezwa na Vyama na Shirikisho. | Taarifa za afua zilizotekelezwa | Shirikisho, Vyama na Serikali |
| **Ufanisi wa Mipango ya Maendeleo inayotekelezwa na Vyama** | Idadi ya mipango ya maendeleo iliyobuniwa na kutekelezwa | Taarifa za utekelezaji wa mipango ya maendeleo | Vyama, Shirikisho, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Mafunzo ya Usimamizi wa Miradi na Fedha** | Idadi ya Vyama vilivyopata mafunzo ya usimamizi wa miradi na fedha | Taarifa za mafunzo yaliyotolewa | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Kuondoa Vikwazo vya Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu Wenye Ulemavu** | Idadi ya mada zilizotolewa za kuondoa vikwazo vya kimtizamo | Masuala yaliyowasilishwa katika mada | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| | Idadi ya miundombinu fikivu | Taarifa za matokeo ya tathmini ya vikwazo vilivyopo | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Kuimarisha Ushirikiano na Wadau** | Idadi ya vikao/ warsha/ semina / makongamano ya wadau | Taarifa za utekelezaji | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Kujenga Uwezo wa Viongozi wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu** | Idadi ya viongozi waliopata mafunzo | Taarifa za mafunzo | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Maadhimisho** | Idadi ya maadhimisho yaliyoadhimishwa | Taarifa ya maadhimisho | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |
| **Utoaji wa Taarifa** | Idadi ya taarifa zilizotolewa kuhusu utekelezaji wa mwongozo | Taarifa za utekelezaji wa Mwongozo | Shirikisho, Vyama, Wadau wa Maendeleo na Serikali |

**OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

Mtaa wa Kazi, Mji wa Serikali - Mtumba.

S.L.P. 2890 | 40411 Dodoma - Tanzania

+255 26 2963 450/51

+255 26 211 2054

ps@kazi.go.tz

www.kazi.go.tz